JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Nyerere
S.L.P 377 Musoma
Simu: 028-2623029 Nukushi :028- 2623030
Barua pepe: rbcmara@pccb.go.tz
Wavuti www.pccb.go.tz

MARA – APRILI 30, 2020

TAARIFA KWA UMMA

KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu wana Habari,

Mtakumbuka kuwa kwa takriban miezi minane sasa TAKUKURU Mkoa wa Mara imekuwa katika mapambano makali dhidi ya wakopeshaji umiza ambao kwa sehemu kubwa wamekuwa wakiwadhulumu wastaafu na hasa walimu; katika vita hivi tulifanikiwa kuwarejeshea baadhi ya wastaafu waliofika ofisini kwetu fedha walizokuwa wameporwa.

Aidha tumekuwa tukipambana na baadhi ya viongozi wa AMCOS kuhakikisha kuwa malipo ya wakulima kwa mazao waliowakopesha yanalipwa.

Ndugu wana Habari,

Kwa kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020, TAKUKURU mkoa wa Mara iliendelea na uchunguzi wa malalamiko saba (7)ya wakopeshaji umiza yakihusisha jumla ya **shilingi 232,400,000/= nyumba moja** yenye thamani ya **shilingi 55,000,000/= pamoja na tuhuma nane zilizohusu AMCOS.**

Aidha ofisi yangu iliendelea na uchunguzi wa wakopeshaji umiza uliohusisha kujipatia gari moja aina ya TOYOTA NOAH pamoja na tuhuma zingine zlizohusu utakatishaji fedha, ukwepaji wa kulipa kodi pamoja na matumizi mabaya ya ofisi.

Ndugu wana Habari,

Katika malalamiko hayo saba, mawili yanawahusu wastaafu wawili ambapo mmoja alikopa fedha kiasi cha shilingi **1,400,000/=** ili alipe **shilingi 3,000,000/=.** Lakini cha kushangaza, Pensheni yake ya kiasi cha **shilingi 99,000,000/=** ilipotoka, mstaafu huyo akajikuta anaporwa jumla ya **shilingi 86,000,000/=** sawa na **86.9%** ya Pensheni yake - huku riba ikiwa ni 6,143%.

Kwa mahesabu haya, ina maana kuwa Pesheni ya Mstaafu huyu ya **shilingi 99,000,000/=** aliyoifanyia kazi kwa zaidi ya miaka 30 aliambulia **shilingi 13,000,000/=** tu.

Ndugu wana Habari,

Tuhuma hii tumeifanyia kazi na TAKUKURU mkoa wa Mara imefanikiwa kurejesha kiasi cha **shilingi 37,000,000/=** ambazo leo tutamkabidhi mstaafu, na kiasi kilicho baki tutaendelea kukifanyia kazi.

Ndugu wana Habari,

Tuhuma ya pili ambayo bado tunaendelea kuifanyia kazi inamhusu Mstaafu wa pili ambaye uchunguzi wetu unaendelea. Yeye Pesheni yake ilkuwa ni **shilingi 59,000,000/=** na alikuwa na mikopo miwili kwani alikopa kutoka kwa wakopeshaji umiza wawili kwa viwango tofauti.

Mkopeshaji mmoja alimkopesha **Tsh 1,200,000/=** ili amlipe **shilingi 3,000,000/=** sawa na riba ya **250%.** Lakini Pensheni yake ilipotoka mkopehaji huyo akachukua **shilingi 30,000,000/=** sawa na riba ya **2,500%.**

Mkopeshaji wa pili alikuwa amemkopesha shilingi **6,000,000/=**, lakini Pensheni ilipotoka mstaafu huyu akajikuta anaporwa **shilingi 25,000,000/=** sawa na **417%.**

Ndugu wana Habari,

Kupitia uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Mara, wakopeshaji hawa wamekubali kuwahi kuwa na uhusiano wa kiukopeshaji na mwalimu huyu mstaafu (ambaye pia ni mlemavu), ila wamekana kutoa mikopo hiyo kwa viwango hivyo.

Ofisi yetu ya mkoa wa Mara bado inaendelea na uchunguzi ila kwa leo mstaafu huyu atarejeshewa kiasi cha **shilingi 11,000,000**/= kama sehemu ya marejesho yaliyofanywa na Wakopeshaji umiza baada ya TAKUKURU kuingilia kati.

Ndugu wanaHabari,

Kesi nyingine ambayo TAKUKURU mkoa wa Mara iliwahi kuitolea taarifa ni ile inayohusu watumishi wa Serikali kuwa MAWAKALA wa WAKOPESHAJI. Watumishi hawa ni MAKATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU ambao katika tuhuma nne tulizozipokea tumefanyia kazi tuhuma moja na tumethibitisha uhusika wao.

Katika tuhuma hii, Katibu huyo wa Tume ya Utumishi wa Walimu, alibeba hundi ya mafao ya mstaafu kutoka mkoani Mara hadi Mwanza katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando ambako mstaafu huyo alikuwa amelazwa kwa matibabu na alikuwa hawezi hata kutembea.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Mara ulibaini kuwa, mtuhumiwa huyo – mtumishi wa Serikali, alishughulikia kibali cha kumtoa Mstaafu Hospitalini ili wampeleke benki moja wapo Jijini Mwanza, tena nje ya muda wa kazi kwa taratibu za kibenki na kumpora kiasi cha **shilingi 13,000,000/=** ambazo katika kuficha ukweli, fedha hizo zikaingizwa katika akaunti ya mkopeshaji.

TAKUKURU mkoa wa Mara tumeifanyia kazi tuhuma hii na leo hii japokuwa mstaafu Yule bahati mbaya alishafariki, tunamrejeshea mjane wa mstaafu huyo kiasi cha **shilingi 13,000,000/=** baada ya kufanikiwa kuziokoa kutoka kwa Katibu huyo wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Ndugu wanaHabari,

Mstaafu mwingine ni ambaye alikopa shilingi 2,000,000/= ili arejeshe shilingi 4,000,000/=. Lakini Pesheni yake ilipotoka akajikuta amelipa shilingi 13,000,000/= sawa na asilimia 670%.

Hivyo, kwa kifupi siku ya leo TAKUKURU mkoa wa Mara inafanikiwa kurejesha kiasi cha shilingi **74,400,000/=.** Kiasi hiki cha fedha kinafanya jumla ya fedha ambazo TAKUKURU mkoa wa Mara imefanikiwa kukirejesha kufikia shilingi **159,000,000/=** kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Ndugu wanaHabari,

Kufuatia tuhuma za baadhi ya mahakimu kushirikiana na wakopeshaji wasio na vibali leo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Mara imewafikisha Mahakamani Hakimu Mkazi Wilaya ya Tarime Mheshimiwa BHOKE CHACHA KUBYO kwa kosa la kuomba na kupokea hongo ya shilingi 2,000,000/= kutoka kwa mkopeshaji umiza ili amsaidie kufungua **kesi hewa** mbili za madai na kumpa upendeleo katika kesi hizo.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Mara ulibaini kwamba kesi hizi ambazo ni za kupika aliziendesha kutokea nyumbani kwake wakati akiwa katika likizo ya uzazi.

Katika kesi hii pia tumemfikisha mahakamani mfanyabiasha BITARA MUSOBA kwa kosa la kutoa hongo ya shilingi 2,000,000/= kwa Hakimu BHOKE CHACHA KUBYO kama asante kwa kusaidiwa kufungua kesi hewa za madai na kupewa ushindi huku akijua kabisa kesi hizo zilikuwa hewa na kwamba jambo hilo ni kosa.

Ndugu wanaHabari,

Kufunguliwa kwa kesi hii ni mwanzo tu wa kuanza kuwapeleka mahakamani wakopeshaji umiza pamoja na mawakala wao ambao ni watumishi wa Serikali, wanaotumia nafasi zao kuwaumiza wastaafu hususani walimu.

Hivi karibuni tunategemea kuwafikisha Mahakamani baadhi ya mawakala na wakopeshaji umiza ambao pia wanaonekana wameshiriki kabisa katika utakatishaji wa fedha.

Ndugu wanaHabari,

Kwa upande wa AMCOS ndani ya kipindi cha miezi mitatu iliyopita ya Januari – Machi 2020, TAKUKURU mkoa wa Mara imefanikiwa kuokoa jumla ya Kiasi cha **shilingi 43.9 Milioni** ambazo tayari zimeshalipwa kwa wakulima.

Ndugu wanaHabari,

Fedha ambazo TAKUKURU mkoa wa Mara imezidhibiti zikiwa njiani kuingia katika mikono michafu ya walarushwa wachache kwa kipindi cha miezi mitatu ni **shilingi 114.6M** na hivyo kufanya jumla ya fedha **ZILIZOOKOLEWA** katika kipindi cha miezi mitatu kufikia **shilingi 163,390,000/=**

Ndugu wana Habari,

Kupitia kwenu, nitoe angalizo kwa watumishi wa umma walio na dhamana ya kusimamia fedha na vitu vinavyoletwa mkoani hapa kwa ajili ya kupambana na gonjwa la CORONA kutozitumia raslimali hizo kwa maslahi yao binafsi.

Aidha waliopewa dhamana ya kusimamia wagonjwa walio katika zuio wahakikishe kuwa wagonjwa hao wanaendelea kuwa katika zuio na kuhakikisha kuwa hawashawishiki kuomba au kupokea hongo ili wawaruhusu kutoka hata kabla ya madaktari kusema vinginevyo. Tunasema hivi kwani tukiendekeza rushwa katika mapambano dhidi ya CORONA – TUTAANGAMIA.

Ndugu wanaHabari,

Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa viongozi wa mwaka 2020, zipo taarifa za baadhi ya watia nia kuanza kupita pita hata kabla ya muda. Nichukue fursa hii kuwataka waache mara moja.

Iwapo tutawabaini, wakiwa katika harakati hizo, tutawakamata bila kujali umri au nafasi aliyo nayo mhusika katika jamii.

ASANTENI SANA KWA KUNISILIKILIZA.

Imetolewa na :

A.J KUHANDA

MKUU WA TAKUKURU

MKOA WA MARA

30.04.2020